SOMO LA 11

MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSU UZIMA WA MILELE (Sehemu ya 2)

“Saa yaja ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.” (Yohana 5: 28 - 29)

KATIKA SOMO LA AWALI tulipitia ufafanuzi na jinsi Biblia inatumia istilahi ya “mortal” – “kinachokufa” na “immortal” – “kinachodumu milele.” Tuliona jinsi istilahi hizo zinavyotumiwa kuwahusu wanyama na binadamu tukirejelea kanuni za uhai. Tuliangalia hapo nyuma, mwanzo kabisa ambapo Biblia yazungumzia matukio ya chanzo cha kifo; na ikaonyesha ya kuwa kile ambacho ndicho kimesababisha mauti kimerithiwa na vizazi vyote. Somo hili lilitamatishwa kwa uchunguzi ulioonyesha ya kuwa ni habari njema ya Biblia TU inayowapa watu matumaini ya kuishi tena kwa masharti fulani. Dhana yoyote ile inayotoa nadharia ya mpito wa moja kwa moja hadi maisha mengine baada ya kifo kwa watu wote ambao wamewahi kuishi haiambatani na ukweli wa maandiko.

Somo hili litaangazia “immortality” – uzima wa milele – SIO WA ROHO, BALI WA MTU MZIMA; na kile ambacho Biblia inazungumzia ili kuupata huu uzima wa milele.

Tunajifunza kuhusu uzima wa milele katika shughuli zetu za kila siku za hali yetu ya kufa, kufa kabisa kwa kukosa uhai. “Cha kufa” ni kiumbe ambacho chaweza kufa, ambapo maumbile yake ni kifo; anayekufa; hatima yake ni kifo. Twashuhudia haya yalivyotuzunguka kila siku. Maandiko (na sisi wenyewe) huzungumzia kifo cha mnyama kama tunavyozungumzia kifo cha mwanadamu anapoaga. Hatuna tashwishi katika kukubali maana iliyo wazi kwa mnyama. Lakini tukiwa chini ya kongwa la nadharia ya “immortal-soul” – “roho isiyokufa kabisa,” adhabu ya moto wa milele”, tunapomrejelea mwanadamu anayekufa, itamlazimu kupeana neno “kufa” maana nyingine kabisa.

Uzima wa milele ni kinyume tu cha kufa; hali ya kifo, mwisho usio na kikomo. Kuwa na uzima wa milele, twahitajika tuwe watu wasioweza kuharibika (miili yetu), kama ambavyo miili yetu huchakaa. Paulo alipokuwa akizungumzia miili ya wenye haki, ya sasa na ya siku za usoni, katika hali ya mauti na ufufuo, alisema:

“Hupandwa katika uharibifu; hufufuliwa katika kutoharibika … hupandwa MWILI wa asili; hufufuliwa MWILI wa roho” (1 Wakorintho 15: 42 - 44).

Vifungu zaidi 51 - 53 –

“Hatutalala (kufa) sote, lakini sote tutabadilika … Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa.”

Hii ndiyo njia ya pekee ya kufikilia uzima wa milele: kwa mwili kubadilishwa wakati wa ufufuo siku ya mwisho. Hadi wakati huo, wafu “wanalala.”

Angalia kwa makini ya kuwa Maandiko yanatilia mkao wa MWILI.

Hayajui chochote kinachoishi pasipo mwili. Na huu “MWILI wa roho” ni mwili halisi unaoweza kushikwa na kuguswa. Tunaambiwa ya kuwa, miili yetu, itafanywa kama “MWILI wa utukufu” wa Kristo. Twajifunza kuwa haya ndiyo yaliyofanywa kwake baada ya ufufuo wake. Aliwaambia wanafunzi wake:

“Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi MWENYEWE: Nishikenishikeni; mwone; kwa kuwa roho (kama walivyofikiria, ati ni mzimu) haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo” (Luke 24:39)

Kristo aliye na mwili wa kutokufa baada ya kufufuka , alikuwa na “mwili na mifupa.”

“Ni mimi mwenyewe” Wanafunzi walimshika Yesu, na akala nao (k 43). Alimwambia Tomao baadaye (Yohana 20:27)

“Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono uutie ubavuni mwangu. Wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye.” Uu huu mwili ni wa kudumu milele –

“Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni.” (Matendo 1:11). Ni “Yesu huyu” yupi? Yule yule aliyekuwa na “mwili na mifupa” – “Mimi mwenyewe” – waliye – mshikashika siku chache zilizopita. Huu ndio mwili utakaofanyika kama vile wa Kristo wakati wa kurudi kwake, tukimpokea.

Miili ya nyama, au miili hii ya asili, yaendelezwa kwa damu katika mishipa yake:

“Uhai wa mnyama, hiyo DAMU yake ni moja na uhai wake” (Walawi 17:14).

SIO, twaona hapa, sio kitu kinachofikirika tu, kisichoeleweka, chenye cheche ya uzima wa milele au isiyoweza kufa ambayo imevaa tu huu mwili. Maisha ya mnyama ya sasa sio ya asili na ya kujitegemea. Inategemea kuendelezwa kwa kazi ya mwili bila misukosuko yoyote – kupumua, kusaga chakula, uzungungaji wa damu, n.k. – na inategemea mazingira hasa: joto, baridi, ukosefu wa hewa, sumu, maradhi, fujo, ajali, na hii inaweza kuharibu mambo. Na imerithishwa, yenyewe, ikielekea kwenye mauti. Daktari mtaalamu hawezi kuponya hali hii; aweza tu kuahirisha ushindi wa kifo kwa muda mfupi.

Yesu tu ndiye daktari wa kweli anayeponya milele. Yuko tayari na ufufuo ili upatikane mwili wa roho, usiotegemea mazingira, na usiopatikana na ajali, kuyeyuka, maradhi au uharibifu –

“Kilichozaliwa kwa Roho ni roho” (Yohana 3: 6)

-“Wa kufa na kuharibika” “uvae” – umepata “kutokufa na kutoharibika” (1 Wakorintho 15:53).

Paulo aliwambia wale wa eklezia ya Roma (Warumi 8:11) –

“Aliyemfufua Yesu katika wafu (Mfano na mtangulizi) ataihusisha na miili yenu iliyo katika hali ya KUFA kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.”

Angalia vema, uzima wa milele unapatikana kwa MWILI wa kufa kwa “kuhuisha” – SIO kwa chembe fulani kuruka mahali kutoka kwa kitu kisichokufa kabisa kutoka mwilini mwa mtu.

Hali hii ya “kuhuisha” (iliyo na maana ya “kufanya hai”) ni kuzaliwa mara ya pili katika maisha halisi. (Kimaandiko, ni “kuzaliwa” mara ya tatu: Kuzaliwa kwa mwanzo ni kule kutoka tumboni mwa mama; ya pili yarejelea kuzaliwa kwa maji ya ubatizo katika Kristo; kuzaliwa kwa tatu ni kule kutoka kaburini kwa kubadilishwa kwa roho wakati wa ufufuo – Yohana 3:5).

Daniel alionyeshwa kuwa wenye haki watapata kung’aa kama mwangaza wa anga ukidhihirisha miali ya Roho wa Mungu (Daniel 12:3)

“Na walio na hekima watang’aa kama mwangaza wa anga; na hao waongozao wengi kutenda haki watang’aa kama nyota milele na milele.”

Na Isaya anaeleza watapewa nguvu na uwezo , karama ya utukufu kutoka kwa Mungu kuwa kama yeye mwenyewe (Isaya 40:28-31)

Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki…Wao wamngojeao BWANA watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai, watapiga mbio, wala hawatachoka, watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia”

Karama hii ya bure kutoka kwa Mungu (maana mtu ambaye angestahili kupata sifa hiyo) bado inategemea masharti ya kuwa watiifu KABISA kwa kutafuta kutenda sawa na mapenzi ya Mungu kwa dhati. Anayotarajia Mungu kutoka kwetu ni kama yale ambayo tunatarajia kutoka kwa watoto wetu. Hatuwatarajii kuwa pasipo lawama, wakamilifu; bali twatarajia – tukitekeleza wajibu wetu vema (kama vile Mungu hufanya) – wanyenyekee na kutii katika upendo kwa uwezo walionao.

Mungu pekee ndiye Hakimu na mwamuzi wa yaliyo haki kwa njia ya utiifu, kama tulivoona katika Warumi 2:7 –

“Wale (na ni wale tu) ambao kwa Saburi katika kutenda mema wanatafuta… kutoharibika, watapewa uzima wa milele.”

“Saburi katika kutenda mema” ni ufunguo – kitu makini, mwendo sahihi katika roho safi –

“Yeye AFANYAYE mapenzi ya Baba yangu … ndiye atakayeingia katika ufalme” (Mathayo 7:21).

“Yeye ASHINDAYE, nitampa kula matunda ya Mti wa Uzima” (Ufunuo 2:7).

“Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuendea huo MTI WA UZIMA” (Ufunuo 22:14)

“Wokovu wa milele kwa watu wote WANAOMTII” (Waebrania 5:9)

“Lakini ukitaka kuingia katika uzima, ZISHIKE AMRI” (Mathayo 19:17)

Vifungu hivi vyaonyesha ni watu fulani tu wanaofuata mkondo fulani wa maisha ndio watakaopata kutoharibika. Angalia kuwa, yasikitisha, hii inaenda kinyume na nadharia inayopendeza mwili (inayojulikana kama “Universalism” – “ishikayo ulimwengu mzima”). Mungu anahitaji upendo na utiifu wa hiari. Kama tulivyokwisha kuona, hiari ya kufanya mapenzi yake ni mzizi wa kusudi lake Mungu kwa viumbe wake. Ni moja kwa moja kwa wale ambao wataokolewa, Maandiko yanawazungumzia wale ambao wataangamizwa. Mstari unaofuatia Warumi 2, kwa mfano, yazungumzia siku hiyo ya mwisho, “siku ya hasira na ghadhabu”

“Na wale wenye fitina, wasiotii kweli, bali wakubalio dhuluma, watapata hasira na ghadhabu; dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu”

Kinyume ni “Universalism” – “Wokovu kwa walimwengu wote,” Biblia yasema kuwa ni wachache sana watakaookolewa –

“Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani; nao waionao ni WACHACHE (Mathayo 7:14)”

“Mchukueni mkamtupe katika giza la nje… Waitwao ni wengi , bali wateule ni wachache” (Mathayo 22:13)

Haya ya ulimwengu mzima kuokolewa ni kujiona bora na kujipandisha juu sana kwa mwanadamu kupita kiasi. Na inaeleweka, maana wanaona tu ile nadharia isiyo na maana, ovyo, isiyo na lengo maalum, na wengi wa wanadamu kuteseka bila kukoma.

Kusudi la Mungu, kama ilivyofunuliwa na Maandiko, sio kumwendeleza kila mwandamu aliyewahi kuishi. Mpango wa Mungu ni kuwakuza wateule, watu wa kiroho, watu wanaopenda mambo yaliyo ya jamii ya kujali mambo ya mbinguni, ya utukufu na ya kuchukua jina la Mungu. Umati wa watu ulimwenguni ni wa kupita tu pasi kuhusishwa na huu mpango wa Mungu. Mungu kwa rehema yake anawaita wote lakini hamlazimishi yeyote. Mnyama- mtu ambaye ni mavumbi na majivu tu asijiinue kwa kujipa umuhimu kupita kiasi. Mungu –

“Achagua watu katika mataifa kwa ajili ya jina lake” (Matendo 15:14).

Yesu anasema , akifafanua wazi HATIMA hizi mbili (Yohana 5:28 -29).

“Saa yaja ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu”

Kwa wengi ambao kasumba ya nadharia za madhehebu imewasakama, “hukumu” kwao ni picha ya moto wa milele. Lakini hukumu hii ni maangamizi, kukataliwa na ni hukumu ya uharibifu wa kabisa kabisa.

“Wataadhibiwa kwa MAANGAMIZI ya milele” (2 Thess 1:9)

Wengine nao wanasema, kama ni maangamizi basi hiyo si “adhabu” – kuwa mtu anafaa kuwa hai ndipo “aadhibiwe.” Hawajawahi kusikia mahakama ikitoa adhabu ya mwisho!

Kutolewa kwa uhai, kunyongwa hadi ufe – ukose kuishi, ndiyo adhabu kali na ya mwisho. Inaondolea mbali waovu katika ulimwengu huu mzuri bila kuwaacha mabilioni ya watu wakitoa sauti za dhiki motoni. Yeyote anayeamini moto wa milele hafai hata kidogo kujuimuishwa katika familia ya Mungu mwenye upendo. Mungu ni mwenye haki lakini mkali, bali si katili kama wale wanajidai ni Wakristo lakini wamesheheni ushirikina wanavyomchukulia. Kusema kweli, kwa walio waovu,Mungu ni “moto ulao” (Waebrania 12:29) – Lakini, kumbuka, ni “moto ulao”; sio moto utesao milele.

“Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu” (Wagalatia 6:8)

- Kifo kinapata kushindwa mwishowe.Waovu mwishowe wanashindwa na kumezwa kwa “mauti ya pili.” Watu wasiofaa kuwa katika uchumi wake Mwenyezi Mungu, wanaondolewa.

“Waovu huacha kusumbua.” (Ayubu3:17)

Mbali na wale watakaokubaliwa, kuna nasaba ya tatu ya watu ambao hawakufahamu mapenzi ya Mungu, wale ambao hawakupata nuru ya Neno lake.

Hawa hawataokolewa kama inavyochukuliwa kwa kawaida. Kama hawa wangeokolewa, basi inakuwa ni hekima kwa mtu kubaki gizani. Ufahamu waweza tu kuwaharibia wao wokovu. Kuhubiri Injili nayo yaweza kuwa jambo la ukatili mkuu, ikiwa ujinga wahakikisha wokovu. Wakatoliki wana mantiki hapa kuliko Waprotestanti, kwani wana sehemu yao ya “limbo.” “Sehemu yenye utata” kwa kesi zenye mashaka. Lakini wote wamekosea. Biblia yadhihirisha ya kuwa:

“Wote waliokosa pasipo sheria watapotea pasipo sheria.” (Warumi 2:12)

Haki iliyokamilika, busara iliyokamilika: hapana utii wala kutotii, kwa hivyo hapana zawadi wala adhabu. Katika mpango wa Mungu. Wote wale wasio na ufahamu wa sheria zake

hawahesabiki kama wanaowajibika. Hawawezi kufufuliwa. Kama Isaya anavyosema, akiwalenga watu wa mataifa waliokuwa wamewataabisha Waisraeli –

“Wao wamekufa, hawataishi; wamekwisha kufariki; hawatafufuka; kwa sababu hiyo umewajilia, na kuwaangamiza, na kuupoteza ukumbusho wao” (Isaya 26:14).

Kwa watu hao hao Yeremia asema:

“Kulala usingizi wa milele” (Yeremia 51:39)

“Mtu aikosaye njia ya busara atakaaa katika mkutano wao waliokufa” (Mithali 21:16).

“Mwanadamu mwenye heshima, iwapo hana akili, amefanana na wanyama wapoteao” (Zaburi 49:20)

“Wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao” (Waefeso 4:18).

“Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani” (Waefeso 2:12)

Watu wote ni wenye dhambi katika hali yao ya asili, ingawa wengi wao ni wajinga na hawaajibiki:

“Dunia yote hukaa katika yule mwovu” (1 Yohana 5:19)

“Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi” (Warumi14:23)

“Mshahara wa dhambi ni mauti” (Warumi 6:23)

“Dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti” (Yakobo 1:15)

Wakristo washukiwa na nadharia yao kuwaokoa wenye dhambi wasiojua lolote kama kundi (hawataki kuwapeleka kwa moto wa milele) inafanya ujinga uwe wenye faida, na inafanya ufahamu kuwa kitu cha kuepukwa kwa kila njia.

Lakini Mungu ni mwenye haki, haki yake imeonyeshwa hapa. Mungu hangewahukumu kwa haki watu ambao hawakuitii amri ambayo hawakuifahamu. Wala haingekuwa haki kuwazawadi kwa jambo ambalo hawakutenda. Kwa hivyo anawatenga. Mafundisho sahihi juu ya kifo , watu wenye mwili kupotea, kama vile wanyama, inatoa suluhisho kwa jinamizi hili la kutisha linaloshikiliwa na wale wanaosema kuwa mabilioni ya watu wanaoteseka bila kikomo ndiyo hatima ya kusudi la Mungu. Mungu mwenye upendo anaweza kufanya jambo kama hili la kupotosha? Huku kungeonyesha kushindwa kwa Mungu kwa hali ya juu!

Uzima wa milele sio wa sasa, walimwengu hawana. Ni kitu ambacho watapewa wale ambao ni wenye haki na watiifu siku za usoni , kwa rehema zake mwenyezi Mungu, siku ya mwisho mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, atakaporudi duniani kutawala.

MASWALI

1. Ni kupitia kwa ujumbe upi uzima na kutokufa itawezekana kwa wanadamu?
2. Ina umuhimu gani kwa nadharia zinazohusu kuisha baada ya kufa?
3. Nini maana ya “immortality”?
4. Nini itafanyika kwa wenye haki walio hai atakapokuja Yesu?
5. Mwili wa roho una asili ipi? Twajuaje?
6. Miili ya asili inaendelezwa vipi katika maisha?
7. Ni watu wa nasaba ipi watakaokataliwa mbele ya kiti cha hukumu?
8. Istilahi ya “Universalism” – “kilimwengu” inahusika na imani ya mafundisho yapi?
9. Nini itafanyika kwa wale wanaojua lakini wanaukataa ukweli, na wale ambao wanaasi mapenzi yake Mwenye Mungu?
10. Nini kitafanyika kwa wale wanaokufa pasipo na kufahamu Mungu au mapenzi yake?
11. Kwa nini Mungu ni mwenye haki kwa kuwaacha wasio na ufahamu – wajinga – kusalia katika makaburi yao na wasiishi tena?